# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE ELEVEN: “Detention Centre”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: FARAHANI AT THE DETENTION CENTRE IN EUROPE**

- **Farahani (m, 19)**
- **Camp officer (m, 45)**
- **3-5 migrants (mainly male, age not important)**

**SCENE TWO: FLORENCE AND LINDA AT CHARLES HOUSE**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**
- **Charles (m, 45)**
- **MRS. MARAGA**

**SCENE THREE: CHIVASI MEETS THE HUMAN TRAFFICKER AT A BUS STATION**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Smuggler (m, 45)**

**SCENE FOUR: AT THE DETENTION CENTRE OVER SUPPER**

- **Farahani (m, 19)**
- **Min. 5 migrants (mainly male, age not important)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu katika makala nyingine ya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Hiki ni kipindi cha 11 kwenye mfululizo wa mchezo wa redio, **"Ardhi ya Ahadi- hadithi kuhusu Waafrika wanaohamia Ulaya".** Katika kipindi kilichotangulia tumefuatilia kwa karibu maisha ya watu watatu, Farahani, Chivasi na Linda wanapokabiliana na suala la uhamiaji Ulaya. Pia, Linda anarudi nyumbani ghafla bila ya kuwaarifu wazazi wala rafiki zake, kisha kuwawandalia rafiki zake karamu ya kukata na shoka kwenye klabu moja ya mtaani. Wakati huo huo, Farahani hatimaye anafaulu kuingia Ulaya pamoja na wahamiaji wengine kwa kutumia mashua ndogo, lakini wanapokaribia ufuo wa bahari wa Ulaya, Mlanguzi wa watu aliyewasaidia kuwasafirisha anadinda na kuwataka waogelee kilomita chache kufika ufuoni. Watu wengi hufa maji katika bahari hii yenye mawimbi makali. Lakini Farahani anapata bahati na kuokolewa dakika za mwisho mwisho na maofisa usalama wa mpakani kutoka shirika la usalama wa baharini Frontex. Je amefaulu? Nini kitakachomtokea? Na je! Chivasi naye anaichukuliaje safari ya kurudi nyumbani ghafla kwa mpenzi wake Linda. Endelea kuwa nasi usikie mengi

zaidi katika sehemu hii ya mchezo **“Kuzuizini ”,** ambapo kwanza tunakutana na Farahani na wahamiaji wengine wasio halali ambao wamefaulu kuvuka bahari na kuingia Ulaya.

**SCENE ONE: FARAHANI AT THE DETENTION CENTRE IN EUROPE**

1. **SFX: METAL BARRICADED DOOR OPENS**

2. **CAMP OFFICER:** **(points out)** Wewe, wewe, wewe hapo,…. na wewe, -ndio wewe..! Mtazuiliwa hapa kuanzia sasa. Mko chini ya Ulinzi na mtapewa vibali vya kumruhusu kukaa hapa kwa muda wa siku 30. Kisha baadaye huenda mtarejeshwa mlikotoka.

3. **SFX: COMPLAINTS AND MURMURS FROM CROWD**

4. **FARAHANI:** **(shocked)** Nini! Hapana? Nafikiri mmekosea! Hapa ni kama jela! Kuna baridi na tumezungukwa na uzio wa seng’eng’e! Kweli sisi wote wanne tutatosha katika chumba hiki kidogo hivi?

5. **CAMP OFFICER:** Ulidhani utapelekwa katika Hoteli ya kifahari? Sikiliza hapa, mmeingia hapa kinyume cha sheria! Kwanza mna bahati mmepata mahali pa kupumzika. Mtabakia hapa hadi pale tutakapo bainisha uraia wenu. Kwa sasa haya ndiyo yatakayokuwa makaazi yenu. Mtazoea tu!

6. **FARAHANI:** Nataka hifadhi ya wakimbizi. Hilo tu! Nimetoka nchi

inayokumbwa na vita huko Mshariki ya kati. Je itanichukua muda gani kupata hifadhi kama mkimbizi?

7. **CAMP OFFICER:** **(cold)** Sijui. Labda mwezi mmoja, miwili… mitatu ..mwaka au hata kumi. Ulitaka kuja Ulaya sivyo? basi hapa ni Ulaya. Utaratibu hapa, kiamsha kinywa ni saa moja asubuhi, chakula cha mchana ni saa saba na cha jioni ni saa kumi na mbili na nusu. Ukichelewa ole wako hakuna chakula kwako. Na usijaribu kutoroka kwani kamera zetu zinawamulika kila wakati. Kuna swali?

**(silence)**

8. **CAMP OFFICER:** Vizuri. Daktari wetu atakuja kuwafanyia uchunguzi wa kiafya. Lakini ningetaka mfikirie kwa makini suala la kutafuta ukimbizi hapa ulaya au kurudi nyumbani. **(orders)** Funga mlango!

9. **SFX: METAL BARRICADED DOOR CLOSES**

10. **FARAHANI:** **(takes deep breath)** Hii si sawa kabisa! Haiwezekani. Sio nilivyodhania kabisa!

**11. NARRATOR:** Farahani haamini anachosikia na kuona. Baada ya kuhatarisha maisha yake kuingia Ulaya, anajikuta chini ya ulinzi mkali akimulikwa na kamera katika chumba kidogo cha gereza wanamosongamana na wahamiaji wengine watatu wasio halali- wote kutoka mataifa mbali mbali barani Afrika. Ofisa anayesimamia kizuizi hicho ni mkali na hana huruma na mtu, kinyume kabisa na alivyodhania. Je nini utakuwa uamuzi wake? Atafanikiwa kuwashawishi maofisa kumpa hifadhi ya ukimbizi? Tutasikia hayo hivi punde tu. Lakini kwa upande mwingine likizo ya Linda umemalizika na anaondoka nyumbani kurudi Ulaya ili kuendelea na maisha yake. Safari hiyo ya ghafla na jinsi alivyojiweka, imewatamanisha sana rafiki zake kuhamia Ulaya. Lakini ni maisha ya aina gani anayoishi Linda huko Ulaya? Hebu twende moja kwa moja hadi nyumbani kwa Charles tusikie mengi zaidi wakati Linda anapokutana na rafiki yake Florence na Charles aliyefunga naye ndoa ili apate kibali cha kufanya kazi Ulaya .

**<u>SCENE TWO: FLORENCE AND LINDA AT CHARLES HOUSE</u>**

**12. SFX: SOFT MUSIC PLAYING IN THE BACKGROUND**

**13. CHARLES:** **(firmly)** Sawa Florence! Siwezi kuendelea kufanya hivi tena! Tosha!

**14. FLORENCE:** **(calm)** Charles, tumekuwa tukifanya hivi siku nyingi! Usijali, kila kitu kitakuwa sawa.

**15. CHARLES:** Hapana, safari hii sioni mambo yakiwa sawa. Hukuwepo wakati walipokuja. Naonekana mjinga

sana!

**16. LINDA:** **(confused)** Samahani sana - Ndiyo mwanzo nimerudi kutoka nyumbani na nimechanganyikiwa kabisa. Kwani nini kinachoendelea hapa? Kuna tatizo gani?

**17. CHARLES:** **(furious)** *Wewe* ndio tatizo! Hungeondoka!

**18. LINDA:** **(surprised)** Samahani? Nilifikiri ndoa yetu ni ya… yaani niko huru kufanya ninachotaka. Au siyo makubaliano hayo Flo?

**19. FLORENCE:** Ndiyo, ndiyo… Charles ana wasiwasi kwa sababu wakati uliposafiri, maofisa wa uhamiaji walimvamia na kutaka kufahamu kwanini umerudi nyumbani bila ya kuandamana na mumeo.

**20. LINDA:** **(now shocked)** Ohh Mungu wangu! Kisha? Walitaka nini? Wamejua kinachoendelea?

**21. CHARLES:** Wanatushuku! Wamegundua kwamba kuna watu wanaofunga ndoa bandia ili kuwasaidia wageni kupata vibali vya kufanya kazi Ulaya. Wanataka twende kufanyiwa mahojiano tena!

**22. LINDA:** Kwa mara nyingine? Florence, sasa nitafanya nini? Sitaki kurudishwa nyumbani. Siwezi!

**23. FLORENCE:** Msiwe na wasi wasi. Hivi ndivyo wafanyavyo kila wakati. Lengo lao ni kumtia uoga ili mjikanganye wakati huo wa mahojiano. Muhimu ni kuonyesha ujasiri na kujiamini wakati huo wa mahojiano. Linda: lazima udanganye kwamba kulitokea jambo la dharura nyumbani!

**24. SFX: MOBILE PHONE RINGS**

**25. LINDA:** Samahani wacha niongee na hii simu faraghani.

**26. FLORENCE:** Hapana Linda! Tunazungumza mambo ya maana hapa. Ongea na hiyo simu hapa hapa. Kisha fanya haraka!

**27. LINDA:** **(takes call quickly)** Hello, Mama? Nimefika salama. Tayari nilikuwa nimekutumia ujumbe, hukupata?

**28. MRS. MARAGA:** **(breaks down in tears)** Linda… ni...

**29. LINDA:** Mama – kwani kuna tatizo?

**30. MRS. MARAGA:** **(controlled weeping)** Ni babako amegongwa na gari!

**31. LINDA:** **(shocked)** Eti nini? Haiwezekani **(crying)** Sasa anaendeleaje Mama? Yuko salama?

**32. MRS. MARAGA:** Yuko mahututi. Madaktari wanasema ni mapema mno kusema endapo atapona au la.

(**silence**)

**33. MRS. MARAGA:** …Linda? Upo?

**34. FLORENCE:** Uko sawa, Linda?

**35. CHARLES:** Umeshtuka! Atazimia huyu! Hebu mshike haraka kabla hajaanguka!

**36. NARRATOR:** Uongo ambao Linda alitarajia kutumia kwa maofisa wa uhamiaji kuhusu safari yake ya kurudi nyumbani bila ya kuandamana na mumewe bandia Charles, sasa umetokea ukweli. Aliposikia babake yu hali mahututi hospitalini alianguka na kuzimia papo hapo. Ilibidi Charles na Florence kumsaidia na kumlaza kwenye kochi. Wakati huo huo, Chivasi anamuwaza sana Linda baada ya viza yake ya kwenda kumtembelea kukataliwa mbali kutokana na sababu kwamba hana pesa za kutosha kwenye akaunti yake ya Benki. Lakini bado anataka kutimiza ahadi yake, na anaamua kuvuka bahari kwenda ulaya kuishi na mchumba wake. Chivasi anaomba likizo kazini na kuabiri basi linalomsafirisha hadi Afrika Kaskazini. Baada ya kusafiri kwa muda wa siku kadhaa, hatimaye anawasili katika ufuo wa bahari wa Afrika Kaskazini, na kukutana na walanguzi wa watu waliomsaidia Farahani kuingia Ulaya. Endelea kusikiliza.

**SCENE THREE: CHIVASI MEETS THE HUMAN TRAFFICKER AT A BUS**

**STATION**

**37. SFX: BUS STATION AMBIENCE**

**38. SMUGGLER:** **(discreetly)** Habari. Wewe ni mkaazi wa hapa?

**39. CHIVASI:** Eeee…Hata. Hii ni mara yangu ya kwanza kuingia nchi hii.

**40. SMUGGLER:** Nini kinachokuleta hapa? Wewe ni mtalii? Hapa si salama kutokana na ghasia za kisiasa zinazoendelea.

**41. CHIVASI:** Nafahamu hilo! Lakini hata nchi ninayotoka pia hali ni hiyo hiyo.

**42. SMUGGLER:** **(excited)** Aha… Kwa hiyo,…bila shaka unataka kusafiri?

**43. CHIVASI:** Kusafiri? Mbona sikuelewi ?

**44. SMUGGLER:** Unataka kuhamia Ulaya?

**45. CHIVASI:** **(timid)** Ndiyo. Unaweza kunisaidia?

**46. SMUGGLER:** Ha haha ! Hapa umefika! Maana unazungumza mwenyewe! Na kisha una bahati sana. Leo kuna meli za mizigo zinayoleta msaada wa chakula cha

wakimbizi kutoka Ulaya. Nina rafiki yangu anayefanya kazi katika meli hiyo, na anasema kuna nafasi ya watu watano. Wewe ndiye mtu wa mwisho.

**47. CHIVASI:** Ah… sawa basi … Kwa hiyo hii meli itanipeleka hadi Ulaya? Lakini zisiwe nii zile mashua ndogo ndogo. Sivyo?

**48. SMUGGLER:** Hata…! Hii ni meli kubwa sana … Meli ya mizigo..! Ni nzuri sana.! Hii itakupeleka hadi katikati mwa Ulaya.

**49. CHIVASI:** Kwa kiasi gani cha pesa?

**50. SMUGGLER:** Euro elfu mbili. Na ni bei nzuri sana. Fikiria kwani hii ni bahati yako imebaki nafasi moja tu.

**51. CHIVASI:** Euro elfu mbili! Hii ni zaidi ya nauli ya ndege kwenda na kurudi Ulaya!

**52. SMUGGLER:** Basi nenda ukasafiri kwa ndege kama unaweza! Unataka nafasi hii ama huitaki? Niko na shughuli chungu nzima.

**53. CHIVASI:** Sawa basi… hizi hapa pesa.…

**54. SMUGGLER:** Hapana ..hapana! Huwezi kulipa hapa! Twende sehemu ya siri. Nifuate.

**55. NARRATOR:** Chivasi anaandamana na mlanguzi huyo wa watu hadi

sehemu ya siri ambako anajiandaa kwa safari yake. Analipa pesa anazohitajika kulipa kisha kusafirishwa kwa mashua ndogo hadi kwenye meli itakayompeleka Ulaya. Anapowasili anaingizwa ndani na kufichwa kwenye sanduku dogo la mbao. Kisha, baada ya saa chache anasikia king’ora cha meli, ishara kwamba safari imeanza. Na muda si muda, Chivasi anajikuta akielekea Ulaya.... Tayari Farahani, yuko Ulaya, lakini mateso yanazidi kumuandama katika jela anamozuiliwa. Jioni hiyo anawaza afanye nini!

**SCENE FOUR: AT THE DETENTION CENTRE DURING SUPPER**

**56. SFX: CANTEEN ATMO**

**57. FARAHANI:** **(addresses fellow migrants)** Sikilizeni hapa kaka na dada zangu!

**58. SFX: METAL PLATE BEING HIT BY SPOON TO DRAW ATTENTION**

**(silence)**

**59. FARAHANI:** Asanteni sana! Wengi wenu hatufahamiani na sijui ni wangapi watanielewa. Japo tumetoka nchi mbali mbali, hiyo si hoja, muhimu hapa ni kwamba sote ni kitu kimoja, tunapitia matatizo sawa. Tumekuwa hapa kwa zaidi ya wiki moja sasa na hakuna mtu anayetuambia mipango inayoendelea.

**60. SFX: LIGHT APPLAUSE WITH CLAPS HERE AND THERE**

**61. FARAHANI:** **(charismatic)** Nafahamu kwamba sote hapa tumeingia Ulaya bila vibali. Lakini sio kwamba sisi ni wahalifu? Sote ni binadamu! Tunachotaka ni kuishi kwa amani!

**62. SFX: MORE APPLAUSE AND SHOUTS**

**63. FARAHANI:** Kwa hivyo, tunachohitaji kufanya ni sote kwa pamoja kususia chakula! Kususia chakula hadi pale kesi yetu itakapoamuliwa kuhusu ombi la kupewa hifadhi kama wakimbizi. Hakuna kula au kunywa. Wangapi wananiunga mkono?

**64. SFX: WILD APPLAUSE NOW FROM MIGRANTS**

**OUTRO:**

Huku wahamiaji hao wakimshangilia Farahani katika kizuizi hicho ndipo tunapofika mwisho wa sehemu hii ya 11 katika mfululizo wa mchezo huu, “**Ardhi ya Ahadi kuhusu Waafrika wanaohamia Ulaya.**” Farahani amefanikiwa kuwashawishi wenzake kuanza mgomo wa kususia chakula hadi kesi zao zitakapoamualiwa kuhusu kupewa hifadhi ya wakimbizi. Je watafaulu? Wakati huo huo, Chivasi amefunga safari ya kuhamia Ulaya bila kibali baada ya kujificha kwenye meli ya mizigo. Mlanguzi wa watu anasema kuwa hii ndiyo njia salama zaidi kufika Ulaya –lakini je asemayo ni kweli? Na ni vipi habari kuhusu hali ya babake itakavyobadili mtazamo wa Linda kuhusu bara Ulaya? Usikose kuungana nasi kwenye kipindi kinachofuata. Pia ukipenda unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu wa dw.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.